**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA** OFISI
**YA WAZIRI MKUU**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**MKOA WA NJOMBE**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA WANGING'OMBE**


***Simu:Mkuu wa Shule 0752002058***

***Makamu Mkuu wa Shule 0753881318***

Shule ya Sekondari Luduga**,**
S. L. P. 88**,** Barua pepe:
ludugasecondary2005@gmail.com **ILEMBULA.**


**KUMB.NA.WDC/JI.V/ VOL.I /2026/2027/01** **13/5/2026**

**Mzazi/Mlezi wa……………………................……………**

**S.L.P.........................................................................................**


**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI <u>LUDUGA</u> HALMASHAURI YA <u>WANGING'OMBE</u> MKOA WA <u>NJOMBE</u> MWAKA 2026/2027.**

**1:0 UTANGULIZI**

Ninafuraha kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika shule hii mwaka **2026/2027.** Shule ya Sekondari Luduga ipo umbali wa km **11** kusini mwa mji wa Ilembula. Ukifika Makambako panda magari yanayoelekea Ilembula. Usafiri wa kutoka Ilembula unapatikana katika kituo cha mabasi cha Ilembula au eneo la hospitali ya Lutheran Ilembula. Nauli ni Tshs 2000/= kwa basi na si zaidi ya shilingi 6000/= kwa boda boda. Watakaotumia usafiri wa mabasi washukie kibao cha LUDUGA SEKONDARI kilicho karibu na shule.

Muhula wa kuanza masomo utaanza katika tarehe itakayotangazwa na serikali. Utatakiwa kuripoti shuleni tarehe hiyo BILA KUKOSA. Zingatia muda wa kuripoti ni kuanzia saa 1:30 asubuhi hadi saa 12:00 jioni**.**

Soma sheria za shule kwa umakini mkubwa na jaza fomu za ahadi za utii wa sheria za shule, fomu ya taarifa binafsi za mwanafunzi na fomu ya kupimwa afya. Fomu hizi ziletwe shuleni zikiwa <u>ZIMESHAJAZWA</u> pamoja na faili lako siku ya kuripoti**. KARIBU SANA**



**2:0 MICHANGO YA SHULE**

| NA | AINA YA MCHANGO | KIASI |
|---|---|---|
| 1 | Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 2 | Tahadhari | 5,000/= |
| 3 | Nembo ya Shule | 5,000/= |
| 4 | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **JUMLA** | **80,000/=** |

Lipa fedha hii kwenye Akaunti Namba **60301000019** NMB, jina la akaunti ni **LUDUGA SECONDARY SCHOOL**. Tafadhali, **HATUPOKEI FEDHA TASLIMU SHULENI** wala kwa **M-PESA** badala yake tuletee RISITI uliyolipia benki au kwa Wakala wa benki. Kwenye risiti hiyo andika jina la mwanafunzi, kidato chake na mchepuo wake. Uongozi wa shule **hautahusika kabisa** kwa upotevu wowote wa fedha itakayolipwa mkononi au kwa M-PESA.

**3:0 SARE ZA SHULE.**

**3:1 WASICHANA**

**a) Sare ya darasani.**

i. Sketi mbili rangi ya kijivu (kitambaa **esteem namba moja**), **ziwe ndefu hadi chini, zisionyeshe sehemu yoyote ya miguu yake na ZIGUSE viatu vyake**. Marinda boksi yawe 10. Rinda boksi kubwa moja mbele na moja nyuma na marinda madogo manne mbele na manne nyuma

ii. Mashati mawili meupe mikono mirefu iii. Sweta mbili rangi ya light blue .

iv. Viatu jozi mbili vyeusi vya kamba vyenye kisigino kifupi (vinavyotumia kiwi) v. Soksi jozi mbili nyeupe zisizo na maua wala maandishi yoyote..

vi. T-shirt moja ya rangi ya kijivu yenye kola na mfuko upande wa kushoto (Form Six) isiyo na maandishi yoyote.

vii. Singrenti nyeupe mbili viii. Pullnecks mbili rangi ya kijivu

**b) Sare za kazi.**

i. Sketi moj a rangi ya light blue mshono wa rinda boksi kitambaa est eem namba moja.

ii. T-shirt moja rangi nyeusi isiyo na kola wala maandishi yoyote iii. Track suit jozi moja rangi ya kijivu yenye miraba myeupe na isiwe na kofia .

**c) Sare za michezo.**

i. T-shirt rangi nyeupe (ya Real Madrid).

ii. Bukuta rangi nyeupe. iii. Raba rangi nyeupe au nyeusi.
iii. Soksi ndefu hadi magotini(stokeni)rangi nyeupe au nyeusi jozi mbili

**d) Kwa watakaovaa hijabu.**

i. Darasani juba rangi nyeupe inayoishia kifuani.Isiwe na maandishi wala mapambo
ii. Kazini juba rangi nyeusi inayoishia kifuani. Isiwe na maandishi wala mapambo

**e)Mahitaji ya kijinsi**

i. Nguo za ndani kuanzia sita(06) na kuendelea ii. Taulo za kike kuanzia bunda tano(05) na kuendelea iii. Taiti (tights) kuanzia nne (04) na kuendelea iv. Sidiria au vibana matiti kuanzia tatu (03) na kuendelea v. Vitenge au kanga kwaajili ya kuogea viwili/mbili (02)

**3:2 WAVULANA**

**i. SARE ZA DARASANI .**

a. Suruali mbili rangi ya kijivu zenye **turn up, upana wa chini usiopungua inchi 18** na mifuko mitatu (miwili ya mbele na mmoja wa nyuma).
b. Mashati mawili meupe mikono mirefu.
c. Sweta mbili rangi ya light blue.
d. Viatu jozi mbili vyeusi vya kamba vyenye kisigino kifupi (vinavyotumia kiwi.
e. Soksi jozi mbili nyeusi zisizo na maua wala maandishi yoyote.
f. T-shirt moja ya rangi ya kijivu yenye kola na mfuko upande wa kushoto
(Form Six) isiyo na maandishi yoyote
g. Singrenti nyeupe mbili
h. Pullnecks mbili rangi ya kijivu
i. Mkanda mweusi wa ngozi mmoja

**ii. SARE ZA KAZI.**

a. Suruali moja rangi ya dark blue yenye **turn up, upana wa chini usiopungua inchi 18** na mifuko mitatu (miwili ya mbele na mmoja wa nyuma).
b. T-shirt rangi ya nyeusi isiyo na kola wala maandishi yoyote
c. Track suit jozi moja rangi ya kijivu yenye miraba myeupe na isiwe na kofia.


**iii. SARE ZA MICHEZO.**

a. T-shirt rangi nyeupe (ya Real Madrid).
b. Bukuta rangi nyeupe
c. Raba rangi nyeupe au nyeusi

**iv. MAHITAJI YA KIJINSI**

1. Nguo za ndani (boksa) kuanzia tano (05) na kuendelea
2. Bukta rangi nyeusi au light blue kuanzia mbili (02)na kuendelea
3. Vest au singrenti nyeusi kuanzia mbili (02) na kuendelea

**N.B: HURUHUSIWI KUJA NA NGUO NYINGINE ZAIDI YA ZILE ZILIZOAGIZWA, UKIKIUKA AGIZO HILI UTAPEWA ADHABU KALI NA TUTACHOMA NGUO ZOTE AMBAZO HAZITAKIWI MBELE YAKO. SIKU YA KURIPOTI WAVULANA WAFIKE WAKIWA WAMEVAA TRACK SUIT YA KIJIVU NA WASICHANA WAVAE SKETI YA LIGHT BLUE NA T-SHIRT NYEUSI.**




**3:3 MAHITAJI MENGINE MUHIMU KWA KILA MWANAFUNZI.**

Hakikisha unakuja na vitu vifuatavyo;

i. Godoro **$2^{1/2}$ x 6.**

ii. Sanduku madhubuti (Tranka) la kuhifadhia vifaa vyako

iii. Mashuka mawili; rangi ya Pink (kwa Wasichana) na rangi ya Light blue (kwa Wavulana).

iv. Blanketi moja na chandarua kimoja. Ukubwa wa chandarua uzingatie ukubwa wa vitanda vya shule na godoro

v. Taulo moj a la k u ogea rang i yoy ot e . vi. Ndoo za lit a 1 0 mbili; moj a ran gi y a blu e na ny ing ine rang i ya k ij ani kwa ajili ya kuogea na kuhifadhia maji ya kunywa.

vii. Ndala za kuogea pea moja. Yebo yebo haziruhusiwi viii.
Toilets papers kuanzia bunda tano (05) na kuendelea ix.
Kikombe cha kuogea, dodoki na sabuni za kutosha

x. Dawa ya meno, mswaki, kitana na brashi ya kufulia xi. Mafuta mgando ya kupaka ya kutosha. Vipodozi haviruhusiwi

xii. Vyombo vya chakula: sahani, bakuli, kijiko na kikombe (vyote viwe vya aluminium). xiii. Ream mbili(2) za karatasi (A4) kwa mwaka

xiv. Madaftari makubwa (counter books) 3quire ya kutosha kwa masomo yake yasiyo pungua kumi na tatu(13) au zaidi.

xv. Kalamu za wino mweusi au bluu za kutosha xvi. Kalamu za risasi na rula xvii. Kamusi ya Kiingereza kwa Kiingereza moja xviii. Mafaili mawili (box files) kwa ajili ya kutunzia taarifa zako ofisini. . xix. Mathematical set (mkebe), peni za kutosha penseli na rula. xx. Scientific calculator kwaajili ya somo la **Geography.**

xxi. Tochi au taa moja ya mkononi inayotumia betri au nishati ya jua kwaajili ya matumizi ya dharura umeme ukikatika

xxii. Baadhi ya vitabu kwa kila somo la tahasusi

xxiii. Kila mwanafunzi aje na nakala ya **matokeo yake** ya kidato cha nne(Result slip) na nakala ya **cheti chake cha kuzaliwa.** Mwanafunzi **HATAPOKELEWA** bila kuonyesha nyaraka hizo kwanza.

xxiv. Kila mwanafunzi aje na mfagio laini (soft broom ) mmoja na squizer moja kwa ajili ya kukaushia sakafu.

## 4:0 SHERIA ZA SHULE

**SEHEMU A: MAMBO YAMPASAYO MWANAFUNZI AYATEKELEZE KIKAMILIFU (DO's) 1.** Kufuata vema ratiba ya shule kwa kuamka mapema na kukimbia mchakamchaka, kufanya usafi binafsi na wa mazingira ya shule, kuhudhuria mihadhara ya kawaida na ya dharura, kuhudhuria vipindi vyote vya masomo darasani, kushiriki shughuli nyinginezo za shule baada ya vipindi vya darasani, kushiriki sala za jioni na kuhudhuria maandalio ya jioni (Evening Preparation). Thamini muda kwa kila jambo liliopo kwenye ratiba

2. Kuwa mfano bora wa heshima na tabia njema popote alipo. Hii ni pamoja na kusalimia kwa heshima, kuwaheshimu watu wote(walimu, wafanyakazi wasio walimu, wazazi/walezi, viongozi mbalimbali wa dini na serikali na wanafunzi wenzako)na kuheshimu Bendera ya Taifa, picha za viongozi wa serikali, wimbo wa taifa, nembo ya taifa na fedha za taifa

3. Kukaa kimya muda wote awapo darasani na kutotoka nje bila ruhusa ya mwalimu au kiongozi wa darasa lake

4. Kuvaa sare husika na iliyoruhusiwa wakati wote mwanafunzi awapo ndani na nje ya shule. Wakati wa safari kuja shule au kurudi nyumbani wakati wa likizo ni lazima kuvaa sare ya shule na kitambulisho cha shule. Wakati wa michezo vaa sare za michezo, wakati wa kazi za mikono vaa sare ya kazi na wakati wa darasani vaa sare ya darasani. Kuvaa kofia, mapambo yoyote, kusuka nywele au kuweka dawa, kupaka rangi, kunyoa kipara au panki, kuchonga nywele na kufuga ndevu na kucha/kuweka kucha bandia SI **SEHEMU YA SARE YA SHULE** 5. Kuwahi kurudi shuleni kwa tarehe iliyopangwa kufungua shule. Wachelewaji watachukuliwa hatua sambamba na kuletwa na wazazi/walezi wao.Vinginevyo hatapokelewa shuleni kuendelea na masomo akija peke yake

6. Kuitika kwa haraka wito wa dharura na wa kawaida na kukimbilia aliko mtu anayekuita au unapotakiwa kukusanyika. Hii ni pamoja na kutoa taarifa ya viashiria vyovyote vya uvunjifu wa amani na hatarisho la usalama wa wanafunzi na mali zao, watumishi wa aina zote na mali zao na mali za shule

7. Kusimama katika mistari wakati wa kupokea huduma mbalimbali yakiwemo matangazo, chakula au vifaa vya kazi

8. Kunyoosha mkono unapouliza au kujibu maswali

9. Kuzingati usafi wa mwili, mavazi, mabweni, madarasa na mazingira yote ya shule. Kila mmoja ashiriki mahali anapopangiwa kufanya usafi na kuzingatia usafi binafsi

10. Utunzaji na utumiaji mzuri wa mali za shule zitumiwazo kwa shughuli za shule mabwenini, ukumbini, madarasani, ofisini na mahali penginepo. Mali binafsi za wanafunzi wenzako zithaminiwe na kutunzwa. Uharibifu wowote wa mali za shule au za binafsi lazima ufidiwe na aliyeharibu.

11. Kuwasiliana na wazazi/walezi kwa kutumia simu za walimu walioteuliwa kwa kazi hiyo tu.

**SEHEMU B: MAKATAZO MAKUU KWA MWANAFUNZI (DON'Ts)**

1. Kutotumia lugha mbaya kwa walimu, wazazi/walezi, wafanyakazi wasio walimu, wanafunzi wenzake na jumuiya nyingine nje ya shule
2. Kutotumia madawa ya kulevya ya aina zote wala kuvuta sigara
3. Kutokumbatia uchafu kwa kufuga kucha ndefu, nywele ndefu, ndevu na kuvaa mavazi yasiyo ya heshima. Hii ni pamoja na kushona sare kwa kutozingatia maelekezo ya kujiunga na shule (mfano, suruali za kubana kwa wavulana au sketi fupi kwa wasichana)
4. Kutotoka nje ya mipaka ya shule bila kibali cha mamlaka za shule
5. Kutotembelea nyumba za wafanyakazi wa shule, vilabu vya pombe na baa, majumba ya starehe na nyumba za kufikia wageni (Guest Houses).
6. Kutofanya maongezi yoyote na mzazi/mlezi bila kibali cha mamlaka za shule na katika siku zisizoruhusiwa. Hii ni pamoja na kutotumia maeneo ya nyumba za ibada kama sehemu za wazazi/walezi kuonana na wanafunzi, kuongea nao na kuwapa baadhi ya vyakula visivyoruhusiwa kwa mwanafunzi.
7. Hairuhusiwi kabisa kubadili dini bila IDHINI YA MZAZI/MLEZI na kwa maandishi.
8. Kutoleta shuleni chakula cha aina yoyote kutoka nje ya shule

**SEHEMU C: MAKOSA MAZITO YANAYOWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE MOJA KWA MOJA BILA HATA KUPEWA ONYO LOLOTE**

1. Wizi wa aina yoyote ile
2. Uasherati, ubakaji,ushoga/usagaji(mapenzi ya jinsi moja) na ugoni
3. Ulevi wa pombe aina yoyote ile na uvutaji wa sigara
4. Matumizi ya madawa ya kulevya kama vile bangi, mirungi, cocaine, kubeli n.k
5. Kushtakiwa kwa makosa ya jinai
6. Kupiga au kupigana
7. Kupata au kusababisha mimba ndani na nje ya shule. Bunge la Jamhuri ya Muungani wa Tanzania bado halijafuta Sheria ya Elimu Na.25 ya mwaka 1978 pamoja na marekebisho yake na kanuni zake ambazo ndiyo Msingi Mkuu wa uanzishaji na uendeshaji wa shule zote nchini.
8. Kuharibu kwa makusudi mali ya shule au ya mtu binafsi
9. Kuoa au kuolewa
10. Kutoa au kumsaidia mtu mwingine kutoa mimba
11. Kudharau Bendera ya Taifa, wimbo wa taifa au fedha ya taifa
12. Kugoma, kuchochea na kuongoza au kuvuruga amani na usalama wa shule au watu
13. Kukataa adhabu kwa makusudi
14. Kuwa na simu ya mkononi au vipuri vya simu kama vile betri, "headphone", laini au kasha la simu.
15. Kufanya jaribio la kujiua au kutishia kuua au kunywa sumu

16. Kushiriki au kuendeleza imani za kishirikina shuleni.

17. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro wa muda mrefu

18. Kufanya au kumfanyia mtu biashara yoyote ile shuleni

19: Kumiliki vilipuka na vilipuzi(explosives) kama vile viberiti, baruti na kemikali zinazowaka kwa haraka

20. Kutumia pasi ya umeme, birika la umeme, heater au redio

**NB:** Mzazi/Mlezi na mwanafunzi yafaa kuketi pamoja na **<u>kuzitafakari sheria hizi kikamilifu</u>** na kumuasa mwanao kadri ya unavyoifahamu tabia yake ili aanze kujifunza kubadilika na kuendana na sheria hizi, kinyume na hapo **<u>atafukuzwa shule</u>**

FOMU ZA AHADI ZA UTII WA SHERIA ZA SHULE

(***Ijazwe kikamilifu na mwanafunzi na mzazi/mlezi na kuhifadhiwa kwenye faili binafsi la mwanafunzi shuleni***)

**A: AHADI YA MWANAFUNZI KUTII SHERIA ZA SHULE NA KUTOSHIRIKI FUJO, MIGOMO NA MAKOSA YA JINAI**

Mimi………………………………………………wa Kidato cha……………..mwaka 20……..… ninakiri kuwa nimeelimishwa na kuzielewa Sheria za Shule kama zilivyotolewa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuletwa shuleni kuiongoza jumuiya ya shule ya Sekondari Luduga ambayo mimi ni mmoja wao. Naahidi utii wa sheria hizi bila shuruti na kwamba ni hatia kwangu kuzikiuka na kushiriki katika fujo, migomo na makosa ya jinai. Ninakubali kuwa nikizikiuka sheria hizi ninastahili na nitapokea adhabu kwa mujibu wa sheria hizo. Ahadi hii itadumu muda wote nitakaosoma katika shule hii

Sahihi ya Mwanafunzi……………………………………………tarehe………………………..

**B: AHADI YA MWANAFUNZI KUTOMILIKI NA KUTUMIA SIMU NA VIFAA VYAKE AKIWA SHULENI**

Mimi……………………………………………..mwanafunzi wa kidato cha ……… mwaka 20…….

Nimefahamishwa na kuelewa juu ya sheria inayonizuia kumiliki na kutumia simu ya mkononi au vipuri vya simu kama vile betri, "headphone", laini au kasha la simu niwapo shuleni. Nimefahamishwa na kuelewa madhara makubwa yanayoweza kutokea kwa kutumia simu au vifaa vyake shuleni.Naelewa kwamba kuvunja sheria hii ni kosa la **<u>KUFUKUZWA SHULE MOJA KWA</u> <u>MOJA</u>** bila onyo lolote la awali. Nakubaliana na uongozi wa shule kwamba nikitenda kosa hili ninastahili adhabu hii na sitastahili huruma au kukata rufaa kwa mamlaka nyingine yoyote ile.

Ahadi hii itadumu kwa muda wote nitakaosoma katika shule hii.

Jina la mwanafunzi………………………………sahihi……………………..tarehe……………..

Jina la mzazi/mlezi……………………………….sahihi……………………..tarehe…………….

Namba ya/za simu ya/za mzazi/mlezi inayo/zinazo patikana muda wote…………………………….

**C: AHADI YA MZAZI/MLEZI KUKUBALIANA NA SHERIA ZA SHULE NA MAELEKEZO MENGINE YALIYOTOLEWA KWA MTOTO WAKE.**

Mimi ……………………………………………………….ambaye ni mzazi/mlezi wa mwanafunzi ………………..  …………………………………..wa Kidato cha …………mwaka…………..ninakiri kuwa nimesoma na kuelewa sheria, kanuni na maelekezo ya kujiunga na Shule ya Sekondari Luduga. Ninakubaliana na masharti yote yaliyomo katika maelezo ya kujiunga na shule ikiwa ni pamoja na sheria na kanuni za shule. Ninakubali mtoto wangu kujiunga na Shule ya Sekondari Luduga kuanzia tarehe …………………..... Naahidi kutoa ushirikiano mzuri kwa Uongozi wa Shule ili kuhakikisha mwanafunzi mtajwa hapo juu anafuata sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule bila usumbufu wowote. Nitakuwa tayari kumpokea mtoto wangu wakati wowote endapo atakiuka masharti yaliyomo katika sheria za shule na hivyo kufukuzwa shule. Ahadi hii itadumu kwa muda wote ambao mwanangu atasoma katika shule hii

Sahihi ya Mzazi/mlezi……………………………………………tarehe……………………

---

**FOMU YA MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI**

**A**: 1. Jina laMwanafunzi……………………………………………………………………………………

2. Tarehe ya Kuzaliwa…………………………..…Mwezi………..……Mwaka…….........…………

3. Mahali alipozaliwa: Kijiji/Mtaa/Sharia …………………….........…Kata……………….……….

Wilaya…………………………………………………………………..……..Mkoa……………………………

4.Dini……………………………………………....……..dhehebu……………..........…….…..…………......

**B**:1.Jina la Mzazi/Mleziwa Mwanafunzi……………………………………………………..........…

2. Kazi ya Mzazi/Mlezi……………………………………………………………………………………

3. Anwani ya Mzazi/Mlezi……………………………………………………………….............………

4. Mahali anapoishi Mzazi/Mlezi: Kijiji/Mtaa/Sharia…………………….………Kata...……….……

Wilaya………………….…..……Mkoa…………….…………….Na. ya Simu…………………………………

**C**: Majina ya ndugu wengine wawili tu wanaohusika na malezi ya mwanafunzi huyu

1. Jina la ndugu………………………………………………………………………………………………..

Mahali anapoishi: Kijiji/Mtaa/Sharia ……………………………….……Kata……………………..

Wilaya…………………………………Mkoa………..……………………Na. ya Simu…..……………...……

2. Jina la ndugu………………………………………………………………………………….…....……..

Mahali anapoishi: Kijiji/Mtaa/Sharia………………………………..……Kata……………………

Wilaya…………………….…….Mkoa………………….……………Na. ya Simu…………………………..

**D:** Taarifa za viongozi wa ofisi ambako Mzazi/Mlezi wa mwanafunzi anaishi

1.Jina la Afisa Mtendaji wa Kijiji/Mtaa/Sharia……………………….……………………….....

Jina la Kijiji/Mtaa/Sharia………..………………..…………S.L.P…………………………………………

Sahihi na muhuri ……………………..…..Namba ya simu……………………………………………

2..Jina la Mwenyekiti wa Kijiji/Mtaa/Sharia…………………………………………………………..

Jina la Kijiji/Mtaa/Sharia ……………………………………………………S.L.P…………………………………

Sahihi na muhuri ……………………………………..Namba ya simu…………………………………………..

**MEDICAL EXAMINATION FORM**

Luduga Secondary School,
P.O.Box 88, **ILEMBULA**

**Date……………………..**

**To the Medical Officer**
**……………………………………..**
**……………………………………..**

**RE: REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**
**(***To be filled by District/Regional Medical Officer and brought to school by the student in his/her first arrival)*
Student's full name…………………………………………..Sex………………..Age………………..
Please examine the above named student as to his/her fitness for full Secondary Education Course
Blood Count (haemoglobin) ___________________________________________
Stool Examination ___________________________________________
Urinalysis ___________________________________________
Venereal diseases ___________________________________________
Eye Test ___________________________________________
T B Test ___________________________________________
Ears ___________________________________________
Asthma ___________________________________________
Speech ___________________________________________
Abdomen ___________________________________________
Blood pressure ___________________________________________
Leprosy___________________________________________
Heart disorders___________________________________________
Neurosis___________________________________________

**ADDITIONAL INFORMATION (If any)** e.g. physical deformity
______________________________________________________________
_____

**MEDICAL CERTIFICATE**

*(To be filled by the examining Medical Officer)*

I certify that the above mentioned student is fit/not fit for full Secondary Education Course
Name______________________Signature______________

Designation ________________________________Date ___________________________

Official Rubber Stamp

**NOTE:** Medical officer should report any impairment noticed at the time of examination of the individual.
You must bring this completed form when you come to school. No any student may be enrolled without certificate of medical examination.

**8:0 MAWASILIANO MENGINE.**

OFISI YA TAALUMA. 0754502263/0753734088

OFISI YA UHASIBU. 0765439529

OFISI YA MALEZI : 0744656327/0621643977/0755723702

NB: PIGA AU TUMA UJUMBE MFUPI ( kueleza shida yako na ujitambulishe)

**9:0 ORODHA YA BAADHI YA VITABU KWA KILA SOMO**

**A: HISTORY**

1. Major Events in African History by Mwaijage or Fr. Kamara
2. How Europe Underdveloped Africa by Walter Rodney
3. Africa in the World History by Nyirenda
4. Advanced History for Secondary Schools Form Five & Six by TIE
5. Essentials in Advanced Level History Paper 1&2 by Salehe Yassin
6. Contemporary History by Shibitary
7. Modern World History by Ben Walsh
8. The Making of Modern Africa

**B: KISWAHILI**

**KISWAHILI 1**

1. Nadharia ya Kiswahili Kidato cha 5 na 6 –by Nyambari na Masebo (2010)
2. Sarufi maumbo ya Kswahili Sanifu (SAMAKISA) Sekondari na Vyuo –by Kihore et al (2003)
3. Kamusi ya Kiswahili Sanifu- by TUKI
4. Sarufi ya Kiswahili Sekondari na Vyuo (Mdee)-DUP DSM
5. Nadharia ya Lugha Kidato cha 5 na 6-by Saluhaya(2016)
6. Kiswahili 2 Kidato cha 5 na 6 - J. Lwendo(2018**)**

**KISWAHILI 2**

1. Nadharia ya Fasihi Kidato cha 5 na 6- by Masebo
2. Tahakiki ya Vitabu Teule vya Fasihi Kidato cha 5 na 6 –by Nyambari na Masebo

**TAMTHILIYA**

1. Kwenye Ukingo wa Thim – by Ebrahim Hussein
2. Nguzo Mama-  na Penina Mhando
3. Morani – by Emmanuel Mbogo
4. Kivuli Kinaishi—by Said Mohamed

**RIWAYA**

1. Mfadhili – by Hussein Tuwa
2. Kufikirika – by Shaaban Robert
3. Usiku Utakapokwisha – by Mbunda Msokile
4. Vuta N'kuvute – by Shafi Adam Shafi

**MASHAIRI**

1. Chungu Tamu- by Theobald Mvungi
2. Kimbunga – by Haji Gora
3. Fungate ya Uhuru – by Mohamed S. Khatib
4. Mapenzi Bora- by Shaaban Robert



**C: ENGLISH LANGUAGE PAPER ONE**

1. English for Advanced Level- by Dr. M. Kadeghe
2. Advanced Learner's Dictionary- by OUP (Oxford University Press)
3. Advanced Level English Language One Form 5 &6 – by Shadrack and James Kinunda
4. English for Advanced Level Students'book From 5- by TIE
5. English for Advanced Level Students'book From 6- by TIE
6. Advanced English Language Form 5 & 6-by John, J. (2012)
7. Advanced Level English: A Practical Approach- by Asheri, N.(2014)
8. Teaching English as a Foreign Language- by G. Broughton et al
9. A Complete English Course for Form 6- by Michael Kadeghe

**PAPER TWO (READINGS)**

**NOVELS AND SHORT STORIES**

1. The Beautiful Ones are Not Yet Born – by Ayi Kwei Amah
2. A Grain of Wheat – by Ngugi Wa Thiong'o
3. His Excellency the Head of State- by Danny Safo
4. Divine Providence – by S.N Ndunguru
5. A Man of the People- by Chinua Achebe
6. Vanishing Shadows – by Namige Kayombo

**PLAYS**

1. I Will Mary When I Want – by Ngugi wa Thiong'o & Mirii
2. Black Mamba – by John Ruganda
3. The Bride – by Austin Bukenya
4. Betrayal in the City- by Francis Imbunga

5. An Enemy of the People- by Henrick Ibsen
6. Lwanda Magere – by Okoiti Omtatah

**POETRY**

1. Selected Poems from East Africa – by TIE
2. The Wonderful Surgeon and Other Poems- by Charles Mloka